

AGIZO

[Imetolewa Chini ya Kifungu Na. 39 cha Sheria ya EWURA (Sura Na. 414 ya Sheria za Tanzania)]

KWA kipindi kirefu sasa kumekuwa na mtindo wa ujenzi holela wa vituo vya kuuzia mafuta (Petrol Stations) ambavyo vimejengwa pasipo kuzingatia viwango vinavyokubalika vya ujenzi wa vituo hivyo nchini.

BAADHI ya vituo vimejengwa kinyume cha sheria karibu na makazi ya watu pasipo kuzingatia usalama wa watu na mali zao huku vingine vikiwa vimejengwa na kuzungushia ukuta ambapo shughuli mbalimbali zisizoruhusiwa kama uchanganyaji haramu wa mafuta zinafanyika.

MFUMO wa uhifadhi na uuzaji wa mafuta ya Petroli unaoruhusiwa kisheria ni, pamoja na mengineyo, kuwa na:

1. Hifadhi kubwa ya mafuta (Depots) ambapo mauzo ya jumla hufanyika (Wholesale);
2. Hifadhi ndogo ya mafuta kwenye vituo vya kuuzia mafuta (Petrol Stations) ambapo mauzo ya reja reja hufanyika (Retail); na

3. Hifadhi binafsi (Consumer Installations) kwa matumizi binafsi (yasiyo ya kuuza) kwenye maeneo ya migodini, mashamba makubwa, viwandani na kadhalika.

KWAMBA kufuatia taarifa kutoka kwa vyanzo mbalimbali vya kuaminika na kufuatia uchunguzi uliofanywa na EWURA imegundulika kuwa:

1. Ujenzi wa baadhi ya vituo vya kuuzia mafuta umefanyika pasipo kufuata viwango katika sekta ya mafuta ya petroli;
2. Shughuli zinazofanyika katika baadhi ya vituo hufanyika kwa kutumia vifaa visivyostahili kama vile matumizi ya pampu za maji kupakua na kupakia mafuta;
3. Baadhi ya vituo havina vifaa vya kuzimia moto na vingine havina mifumo ya kutolea vimiminika vichafu (drainage system);
4. Vituo vya mafuta vyenye mapungufu tajwa hapo juu ndio chanzo au viko hatarini kutumiwa katika uchafuzi na uuzaji haramu wa mafuta machafu; na
5. Taarifa zetu za ukaguzi wa kila mara na malalamiko yaliyopokelewa kutoka kwa wananchi yanathibitisha kukithiri kwa vitendo hivi viovu, ambavyo haviwezi kufumbiwa macho.

HIVYO BASI EWURA inawaagiza wale wote waliojenga vituo vya mafuta vyenye mapungufu tajwa hapo juu:

1. Kusimamisha mara moja shughuli za biashara ya mafuta katika vituo husika mpaka hapo marekebisho yatakapofanywa na wahusika na EWURA kuridhishwa na marekebisho hayo;
2. Kuvunja uzio/ukuta uliojengwa kutenganisha eneo la mbele (forecourt) na eneo la nyuma lenye hifadhi ya mafuta (backyard storage tanks) mara moja; na
3. Kuondoa mara moja matenki ya mafuta ambayo hayajachimbiwa chini na kuunganishwa na pampu za kujazia mafuta kwenye magari (dispensing pumps).

WANANCHI wanaombwa kusaidia EWURA kwa kutoa taarifa kwa njia ya barua, barua pepe, simu au kwa kufika ofisini kuhusu watakaoendelea kukaidi amri hii baada ya tarehe 31 Desemba 2007 ili sheria ichukuwe mkondo wake.

IMETOLEWA chini ya lakiri ya Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Nishati na Maji (EWURA) leo tarehe 4 ya Mwezi Desemba Mwaka 2007.


.....
HARUNA MASEBU
Director General

